Uvuvio wa Biblia – Uthibitisho

na

Ellis P. Forsman

Uvuvio wa Biblia – Uthibitisho

na

Ellis P. Forsman

October 11, 2011

Uvuvio wa Biblia – Uthibitisho

1 Kor. 14:33

Je uvuvio wa Biblia ni kazi ya Mungu mwenyezi?

Uthibitisho unaweza kutoka katika vyanzo viwili: kwa nje na kwa undani. (Tutazingatia zaidi kiundani).

Uthibitisho unaonyesha kwamba Biblia ni uvuvio ya Mungu.

Umoja wa Biblia

Biblia inaonyesha umoja ambao upo katika hali ya mwanadamu na ambao hauwezi kupingwa. Ili kushukuru kikamilifu umoja huo, mtu lazima ajifunze jinsi Biblia ilivyowekwa kwa pamoja.

Iliandikwa na watu arobaini tofauti kutoka katika nadharia ya utembezi wa maisha.

- Petro alikuwa mvuvi.
- Luka alikuwa daktari.
- Mathayo mkusanya ushuru.
- Paulo alikuwa mtengeneza hema.
- Wengine walikuwa wakulima, wafalme, n.k.

Waliandika kutoka katika kila msingi wa mwanadamu unaliwezekana.

- Daudi aliandika kutoka katika marefu ya furaha kwenye gombo, miinuko yenye nyasi ya Judea.
- Paulo aliandika kutoka katika maumivu yaliyo sababiswa na ubaya wa Rumi.

Waliandika kwa lugha tatu (Kiebrania, Kiaramaika, na Kiyunani), kimsingi kutoka katika mabara mawili (Uropa na Asia), zaidi ya muda mrefu hiyo inafunga karibia karne kumi na sita (1500 B.C hadi A.D 100).

Vile vile Biblia bado inashikilia utulivu uliokamilika kwanzia mwanzo hadi mwisho (Kuanguka kwa mwanadamu na kuokolewa kwa mwanadamu, hiyo inaharibu maelezo mengine.

Mfano tukipata watu arobaini tofauti kuandika kwa kujitegemea juu ya somo moja – matokeo yatakuwa ni nini?

Ukweli uliokamili wa Biblia

Biblia ili iwe neno la Mungu lililo vuviwa lazima liwe kamilifu katika somo linalojadiliwa. 1 Kor. 14:33, "*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.*

Nyakati kwa nyakati tena Biblia imekuwa ikipinga lawama zinazoelekezwa dhidi yake.

Musa akiandika torati

Biblia inasema kwamba Musa aliandika torati. (2 Nya. 34:14; Ezra 6:18; Neh. 13:1; Yoh. 5:46; Mk. 12:26).

Wengine wanasema kwamba Musa asingeweza kuandika vitabu vitano vya kwanza vya Biblia, kwa sababu mfumo wa uandishi ulikuwa bado haujaboreshwa hadi baada ya kifo chake. Pia, walidai kwamba sheria aliyoandika ilikuwa yenye kuona mbele.

Wanaakiolojia wana uthibitisho wa kidunia katika mji wa Lachishi, Ras Shamra, Susa (kwa sasa Iran) kwamba maandishi yalikuwepo miaka mia kabla ya wakati wa Musa. Kiunganishi cha Hammurabi, (2,000 – 1700 B.C) iligunduliwa na jopo la wanaakiolojia wa Kifaransa. Iliandikwa katika kipande cha jiwe na ikawa na sheria endelevu iliyofanana na ya Musa.

Sargoni wa Isaya, Mfalme wa Ashuru (Isa. 20:1) alidhihakiwa na waliopinga

Isa. 20:1, "*Katika mwaka ule jemadari yule alipofika Ashdodi, alipotumwa na Sargoni mfalme wa Ashuru naye alipigana na Ashdodi akautwaa.*"

Katika 1843, Paulo Emile Botta, alipindua makazi ya Sargon.

Leo, tani arobaini za mawe zinaonyeshwa katika Chuo cha Chicago huko marekani.

Kitabu cha Luka cha Matendo ya Mitume kilihojiwa

Bwana William Ramsey, mwana akiolojia maarufu wa karne ya kwanza, aliamua kupinga matukio na sehemu ambazo Luka alieleza. Alafu baadaye akakiri kwamba Luka alikuwa sahihi katika kila kitabu alichoandika.

Leo hii, inapokaguliwa, matukio yote, nchi na hata miji imewahi kukutwa ambapo Luka aliposema yapo. (Hata Sergio Paulo mtu mwenye akili wa Cyprus (Mdo. 13:7) amewahi kuulizwa, lakini wanahistoria wamethibitisha kwamba aliishi na alikuwa kiongozi.)

Mdo. 13:7, "*Mtu huyu alikuwa pamoja na liwali Sergio Paulo, mtu mwenye akili. Yeye liwali akawaita Barnaba na Sauli waje kwake, akataka kulisikia neno la Mungu.*"

Wahiti walikuja chini ya macho ya wahakiki wa Biblia

Walisema kwamba hawaja wahi kuishi.

Wanatajwa zaidi ya mara arobaini katika maandiko. (Kut. 23:28; Josh. 1:4; 2 Fal. 7:6).

Wakati wa mwisho miaka ya 1800, A.H. Sayce aligundua maandishi huko Syria yaliyothibitisha kwamba Waashuru waliishi na walikuwa na nguvu. Katika kitabu cha, *Utambulisho wa Jumla wa Biblia,* Geisler na Nix waliandika: "Uhakiki wa Uzuri wa Biblia katika mambo ya kweli yanaleta sifa katika madai yake unapoongelea juu ya masomo mengine."

Unabii wa Biblia

Moja ya uthibitisho wa kindani unaovutia ya uvuvio ya Biblia ni unenaji wake wa kinabii. Ili unabii uwe na sifa lazima itimize baadhi ya matakwa. Lazima ieleweke, maelezo ya kindani yaeleweke, bure, ipingwe kana kwamba ni bure, au kiasili ni jumla.

Lazima kuwe na muda wa kutosha kati ya maelezo ya unabii na utimilifu wake. (Mapendekezo ya ambacho kinaweza kutokea baadaye haina sifa kama kutajwa kwa unabii. Pia, lazima kusiwe na nafasi yo yote ile ya nabii kuwa na uwezo wa kuvutia matokeo.)

Unabii suo lazima iwe na tani nyingi za kihistoria. (Kwa lugha nyingine, unabii wa kweli haupaswi kuegemea katika yaliyopita (au yaliyopo) kijamii au hali ya kiuchumi.)

Unabii wa wazi, unaoeleka, na ulio kamili, lazima iwe na uelewa wa wazi, utimilifu wa hakika. (Haitoshi kupendekeza kwamba tukio fulani

limekuwa kweli kwa kiwango cha juu cha uwezekano. Utimilifu haupaswi kukosewa, na lazima ifanane na unabii katika kila nyanja.)

Angalia haya:

Ezekieli anatabiri kuanguka kwa mji wa Tiro nguvu ya miujiza.

Alitabiri kwamba Nebukadneza, mfalme wa Babeli, angeangamiza mji. Ezek. 26:7-8, "*Maana BWANA Mungu asema hivi; tazama nitamleta Nebkadreza mfalme wa Babeli, mfalme wa wafalme, juu ya Tiro toka kaskazini, pamoja na farasi na magari ya vita, na wapanda farasi na jeshi na watu wengi. Atawaua binti zako kwa upanga katika mashamba; naye atafanya ngome juu yako, na kuiinua ngao juu yako.*"

Mataifa mengi yatakuja dhidi yake. Ezek. 26:3, "*Basi Bwana MUNGU asema hivi; tazama mimi ni juu yako Ee Tiro nami nitaleta mataifa mengi kupigana nawe, kama bahari iinuavyo mawimbi yake.*"

Mji utasawazishwa na kubomolewa kama mwamba ulio wazi. Ezek. 26:4, "*Nao wataziharibu kuta za Tiro, na kuibomoa minara yake, tena nitakwangua hata mavumbi yake yamtoke, na kumfanya kuwa jabali tupu.*"

Mawe ya miji mbao, na udongo vingetupwa baharini.

Historia inaonyesha kwamba kila utabiri huu ulikuwa wa kweli. Tiro, mji wa kati wa nyakati za enzi, pia ilikuwa na kisiwa cha robo tatu ya kilomita hadi ufuoni. Nebukadneza alikabili mji wa bara mwaka wa 586 B.C., alafu hatimaye alipokuwa kuukalia mji ilikuwa kati ya 573 B.C., ushindi wake uliruhusiwa. Alipata kwamba wakazi wa eneo hilo walikimbilia kisiwani. Hii haikudaiwa kwa miaka 241. Mwisho katika mwaka wa 332 B.C., Alexander Mkuu akaukalia mji, lakini bila kumpuzika. Ili afike kisiwani aliwaruhusu majeshi yake yasawazishe miji ya kisiwani, alafu akatumia vifaa hivyo (mawe, mbao, na udongo) kujengea njia ya kupita kuelekea kisiwani – kiasili walitupwa baharini.

Josia kazi ya maisha yake yalitabiriwa (jina lake hata limo katika misemo ya unabii)zaidi ya hapo miaka mamia kabla hajazaliwa

1 Fal. 13:2, "*Basi mtu huyo akapiga kelele juu ya madhabahu, kwa neno la BWANA akasema hivi, angalia mtoto atazaliwa katika nyumba ya Daudi, jina lake Yosia; na juu yako atawachinja makuhani wa mahali pa juu, wanaofukiza uvumba juu yako, na mifupa ya watu itateketezwa juu yako.*"

Agano la Kale lina zaidi ya unabii wa kimasii zaidi ya mia tatu. Na yote yanakutwa kwamba yametimia katika Agano Jipya. Kuzaliwa kwa Yesu

na bikra kulitabiriwa katika Isa. 7:14 na ikakutwa kwamba imetimizwa miaka mamia baadaye katika Mathayo 1.

Isa. 7:14, "*Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara, tazama bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume naye ataita jina lake Imanueli.*"

Hitimisho

Uthibitisho huu unapaswa kuwa zaidi ya kutosha kuthibitisha kwamba Biblia imevuviwa.